



EQUITY BANK (TANZANIA) LIMITED PRIVACY NOTICE

INTRODUCTION

Equity Bank (Tanzania) Limited, is a licensed commercial bank and registered Data Controller. It is committed to protecting personal data as per data protection laws and this Privacy Notice.

COLLECTING INFORMATION FROM YOU

We may collect and process your personal data through information that you provide us such as when you fill out application forms, through our website, through our app, cards and other digital banking platforms, face-to-face and electronic communication (including telephone conversations) in order to provide our services to you.

THE KIND OF INFORMATION WE HOLD ABOUT YOU

We may collect, store, and use the following categories of personal data about you:

- **Personal contact details** such as name, title, addresses, phone numbers, and personal email addresses.
- **Personal information** such as passport photos, Date of birth, Gender, Marital status, employment status, and Next of Kin.
- **Biometric data** such as fingerprints and facial recognition.
- **Financial information** such as transactions, source of income, estimated turnover and financial statements.
- **Copies of your identity documents** such as NIDA, Driving License, Voter's ID and passports, TIN, Business Documents.
- **Information we obtain from third parties**, such as information that we obtain when verifying details supplied by you and information collected from publicly available sources such as BRELA, RITA, Ministry of home affairs, Municipal council, banks, merchants, NIDA portal, credit reference bureau, TRA, and or fraud prevention agencies, etc
- **Other information** about an individual that you or they disclose to us when communicating with us.
- **CCTV footage** and other information obtained through electronic means in our premises.
- **Device and Location Data** such as IP addresses, IMSI (International Mobile Subscriber Identity that identifies a mobile network user on a SIM card), GPS location.

- **Cookies** to operate and provide our services, services that are web-based, improve your experiences, understand how our services are being used, and customize our services

COOKIE STATEMENT

We use cookies to operate and provide our services, including to provide our Services that are web-based, improve your experiences, understand how our Services are being used, and customize our Services. For example, we use cookies to provide Equity Group for web and desktop and other web-based services. We may also use cookies to understand which of our Frequently Asked Questions (FAQs) are most popular and to show you relevant content related to our Services. Additionally, we may use cookies to remember your choices, like your language preferences, to provide a safer experience, and otherwise to customize our Services for you

Please read the section on our website relating to cookies which can be accessed here visiting <http://equitygroupholdings.com/privacy-policy>.

LOCATION INFORMATION

We collect device location information if you use our location features, like when you choose to share your location with your contacts, view locations nearby or those others have shared with you, and the like, and for diagnostics and troubleshooting purposes such as if you are having trouble with our app's location features. We use various technologies to determine location, including IP, GPS, Bluetooth signals, and information about nearby Wi-Fi access points, beacons, and cell towers.

CCTV NOTICE

Please be aware that this area is under 24-hour CCTV surveillance for the safety and security of all visitors, staff, and premises. This is requirement by the Bank of Tanzania, video footage is recorded and monitored in compliance with applicable data protection laws and regulations.

Purpose of CCTV Monitoring

The CCTV system is in place to:

- Deter and detect criminal activities.
- Ensure the safety and security of individuals and property.
- Aid in any necessary investigations.

Data Protection

Your privacy is important to us. All footage captured by CCTV is securely stored, accessed only by authorized personnel, and retained only as long as required by law or operational necessity.

HOW WE USE YOUR INFORMATION

We'll only use your information where we have your consent or where we have another lawful reason including:

- **To Fulfill Contractual Obligations:** To carry out our responsibilities under any agreements made between you and us or to take steps toward forming an agreement with you.
- **To Meet Legal and Regulatory Requirements:** To comply with legal, regulatory, and reporting obligations set by governing authorities.
- **To Provide Services and Manage Accounts and Relationships:** To offer our services to you, manage your accounts, and maintain our relationship with you.
- **To Address Inquiries and Complaints:** To respond to your inquiries, handle complaints, and address any other requests you've made to us.
- **To Inform You About Products and Services:** To keep you updated on the products and services you hold with us and send you information on other products or services (including those from partner companies) that may interest you, unless you have opted out of receiving such updates.
- **To Prevent, Detect, and Investigate Fraud and Other Crimes:** To prevent, detect, and investigate fraud and other alleged criminal activities.
- **To Verify Your Identity:** To protect you and your assets by verifying your identity.
- **For Evaluation and Analysis:** To conduct assessments, tests (including systems tests), and analyses (including credit scoring and behavioral scoring), as well as statistical, market, and product analysis, and market research. [We may use this information to prepare statistical reports to share internally or with our group companies. These reports are compiled from information about you and other customers, but they are never personal, and your identity remains anonymous.]
- **To Enhance and Improve Our Services:** To assess, develop, and improve our services to you and other customers.
- **To Protect Our Business Interests and Develop Business Strategies:** To safeguard our business interests and advance our business strategies.
- **To Communicate with You:** To contact you by post, phone, text, email, and other digital methods. This may include purposes like collecting any outstanding debts owed to us.

AUTOMATED DECISION MAKING

If you apply to us for a product, your application may be processed by an automated decision-making process such as:

- Credit and affordability assessment checks to determine whether your application will be accepted as well as decide credit limits.
- Anti-money laundering and sanctions checks

INFORMATION SHARING

We keep all your personal data confidential. However, in order to service your needs and provide you with the best products and services, we may share any information you provide to us with our group companies and their agents, counterparties and support service or data providers, wherever located. If you have provided information to other members of our group, those entities may also share that information with us. We will ensure that if we share such information with third parties, any such disclosure is at all times in compliance with the law.

To help us provide services, your data will be processed internally and externally by other third parties. We use third parties for [administrative, servicing, monitoring and storage of your data]. We will outsource some services to third parties whom we consider capable of performing the required processing activities so that there is no reduction in the standard of service provided to you by us.

The recipients or categories of recipients of your information may also include:

- **Regulatory authorities** in connection with their duties such as revenue authorities and investigative agencies.
- **Payment partners** who assist us to process money transfers whether locally or internationally.
- **Third-party agencies** who assist us to perform markets surveys.
- **Vendors** who the bank outsources to provide services to support business.
- **Credit reference Bureau**, identity and address verification organizations.
- Anyone to whom we may transfer our rights and/or obligations.
- Any other person or organization after a restructuring, sale or acquisition, as long as that person uses your information for the same purposes as it was originally given to us or used by us (or both).

DETAILS OF DATA TRANSFERS OUTSIDE TANZANIA

Information about you in our possession may be transferred or stored in other countries outside Tanzania for any of the purposes described in this Privacy Notice including countries that may have differing (and potentially less stringent) laws relating to the degree of protection of personal information. It holds that such information can become subject to the laws and disclosure requirements of such countries for any lawful purposes.

When we, or our permitted third parties, transfer information outside Tanzania, we or they will ensure

that it is lawful, consent from the data subject was sought, a permit for transfer was granted by the Personal Data Protection Commission(PDPC) and that it has an appropriate level of protection.

RETENTION AND DISPOSAL OF DATA AND OUTPUT

We will only keep the information we collect about you on our systems or with third parties for as long as required for the purposes set out above or as required to comply with any legal obligations to which we are subject.

We will normally destroy, archive, pseudonymize or erase data after statutory timelines lapse. However, we may retain your information, or information relating to your account after you cease to be a customer for longer than this, provided it is necessary for a legal, regulatory, fraud prevention or other legitimate business purposes.

STORAGE OF YOUR PERSONAL DATA AND DATA SECURITY

All the information you provide to us is stored in our secure servers. Where we have given you (or where you have chosen) a password which enables you to access certain parts of our website, you are responsible for keeping this password confidential. We ask you not to share your password with anyone.

We have put in place appropriate security measures to prevent your personal data from being accidentally lost, used or accessed in an unauthorized way, altered or disclosed.

We have put in place procedures to deal with any suspected data security breach and will notify you and any applicable regulator of a suspected breach where we are legally required to do so.

Please read the section on our website relating to online security which can be accessed here visiting <http://equitygroupholdings.com/privacy-policy>.

OUR COMMUNICATION WITH YOU

We may communicate with you via electronic mail (e-mail), post, phone, text, and other digital methods. We will never ask you for your password or account number.

When you contact us through any of our communication channels, including visiting a local branch or calling the telephone banking service, we will verify your identity by asking you a number of questions based on information known to us about you and the transactions on your account. We may record your calls for training, quality and security purposes.

MARKETING INFORMATION

Equity Bank may contact you about services of interest through various communication channels. You can opt out of such communications at any time by contacting TZ-DPO@equitybank.co.tz or [contact us](#). The bank may verify your identity to ensure privacy and security.

YOUR RIGHTS

You have several rights in relation to the information that we hold about you, including:

- **Right to access** your personal data in our custody, to know the purpose of processing and our third-party processors.
- **Right to prevent collection or processing of your personal data;** We may however continue to process where we have a legitimate reason to do so or required by law.
- **Right to rectification;** to correction of false or misleading data.
- **Right of Erasure;** (right to be forgotten); the right to request that we delete false or misleading data about you. The right to have any information we hold about you deleted; however, we may reject the request if we have legitimate reasons not to or required by the law.
- **Right to object to direct marketing;** you have the right to opt-out of any marketing communication sent to you by calling our contact center or reaching to us through email: dpotz@equitybank.co.tz
- **Right to prevent automatic decision making;** you have the right to be informed of any automatic decision making or profiling done on your personal data to that affects the level of service you receive. You also have the right to object to such processing, you can exercise this right by contacting us through email: TZ-DPO@equitybank.co.tz or [contact us](#)

You have the right to lodge a complaint with Equity Bank or raise a question about this Privacy Notice, Please [contact us](#) on TZ-DPO@equitybank.co.tz or visit any of our branches near you.

THIS PRIVACY NOTICE

The content or services mentioned on our website may be changed in future and consequently this Privacy Notice may also change. Any changes we may make to this Privacy Notice in the future will be posted on this page and where appropriate, notified to you through our various channels.



EQUITY BANK (TANZANIA) LIMITED

TAARIFA YA FARAGHA

UTANGULIZI

Equity Bank (Tanzania) Limited ni benki ya kibiashara nchini Tanzania, ya huduma za kifedha. Equity Bank (Tanzania) Limited imesajiliwa kama Mkusanyaji wa Taarifa binafsi chini ya Tume Ya Ulinzi Wa Taarifa Binafsi na inajukumu la kushughulikia taarifa zako kwa mujibu wa sheria za Ulinzi wa Taarifa Binafsi. Tafadhali soma maelezo yafuatayo kwa uangalifu ili kuelewa taratibu zetu kuhusu taarifa zako binafsi na jinsi tunavyo zitumia.

UKUSANYAJI WA TAARIFA KUTOKA KWAKO

Tunaweza kukusanya na kuchakata taarifa binafsi kwa kutumia taarifa unazotupatia, kama vile unapojaza fomu za maombi, kupitia tovuti yetu, app, kadi na majukwaa mengine ya kibenki, mawasiliano ya ana kwa ana au ya kielektroniki (ikiwa ni pamoja na mazungumzo ya simu) ili kukupatia huduma zetu.

AINA YA TAARIFA TUNAZOWEZA KUHIFADHI KUHUSU WEWE

Tunaweza kukusanya, kuhifadhi na kutumia aina zifuatazo za taarifa zako binafsi:

- **Maelezo ya mawasiliano** kama vile jina, anuani, namba za simu, na barua pepe binafsi.
- Taarifa kama vile picha za pasipoti, tarehe ya kuzaliwa, jinsia, hali ya ndoa, hali ya ajira na jina la mtu wa karibu.
- **Taarifa ya kibayometriki** kama vile alama za vidole na utambuzi wa uso.
- **Taarifa za kifedha** kama miamala, chanzo cha mapato, makadirio ya mauzo na taarifa ya benki akaunti.
- **Nakala za vitambulisho** kama NIDA, Leseni ya Udereva, Kitambulisho cha Mpiga Kura na pasipoti ya kusafiria.
- **Taarifa tunazopata kutoka kwa watu wengine**, kama zile tunazotumia kuthibitisha taarifa ulizotoa, au zile kutoka vyanzo vya umma kama BRELA, RITA, Wizara ya Mambo ya Ndani, TRA, Manispaa n.k
- **Picha za CCTV** na taarifa zingine zinazopatikana kupitia njia za kielektroniki kwenye majengo yetu.
- Anuani za IP, IMSI, mahali ulipo kwa kutumia GPS.
- **Vidakuzi** ili kuendesha na kutoa huduma zetu, huduma zinazotegemea tovuti, kuboresha uzoefu wako, kuelewa jinsi huduma zetu zinavyotumika na kubinafsisha huduma zetu.

Aidha, tunaweza kukusanya na kutumia taarifa kuhusu wewe unapotumia huduma zetu kwa njia ya mtandao, kama vile kivinjari au kifaa unachotumia kuingia kwenye tovuti na majukwaa yetu, jinsi unavyotumia tovuti, pamoja na taarifa za trafiki na mahali ulipo.

VIDAKUZI

Tunatumia vidakuzi (cookies) kuendesha na kutoa huduma zetu, ikiwa ni pamoja na huduma zinazotolewa mtandaoni, kuboresha uzoefu wako, kuelewa jinsi huduma zetu zinavyotumika, na kubinafsisha huduma zetu. Kwa mfano, tunatumia vidakuzi kutoa huduma za Equity Group kupitia tovuti na programu za kompyuta pamoja na huduma nyingine zinazotegemea wavuti.

Pia, tunaweza kutumia vidakuzi kuelewa maswali yanayoulizwa mara kwa mara (FAQs) yanayopendwa zaidi na kukuonyesha maudhui yanayohusiana na huduma zetu. Vilevile, tunaweza kutumia vidakuzi kukumbuka uchaguzi wako, kama vile mapendeleo ya lugha yako, ili kukupa uzoefu salama zaidi na kubinafsisha huduma zetu kwako.

Tafadhali tembelea tovuti yetu kusoma Zaidi kuhusu vidakuzi na matumizi yake kwa kubofya hapa <http://equitygroupholdings.com/privacy-policy>.

JINSI TUNAVYOTUMIA TAARIFA ZAKO

Tutatumia taarifa zako tu ikiwa tuna idhini yako au sababu nyingine ya kisheria, ikijumuisha:

- **Kutekeleza Wajibu wa Kikataba:** Kutekeleza majukumu yetu kutokana na mikataba yoyote iliyosainiwa kati yako na sisi au kuchukua hatua za kuingia katika makubaliano na wewe.
- **Kukidhi Mahitaji ya Kisheria na Udhhibiti:** Kutimiza matakwa ya kufuata sheria na kutoa ripoti kwa mamlaka za udhibiti.
- **Kukupa Huduma na Kusimamia Akaunti na Mahusiano Yetu:** Kutoa huduma zetu kwako, kusimamia akaunti zako na mahusiano yetu na wewe.
- **Kujibu Maswali na Malalamiko:** Kujibu maswali na malalamiko yako kwetu na maombi mengine yoyote ambayo umetoa kwetu.
- **Kukufahamisha Kuhusu Bidhaa na Huduma:** Kukufahamisha kuhusu bidhaa na huduma unazomiliki nasi na kukutumia taarifa kuhusu bidhaa au huduma nyingine (ikiwemo zile za kampuni zingine) ambazo zinaweza kukuvutia, isipokuwa umeonyesha kuwa hutaki kupokea taarifa hizo.
- **Kuzuia, Kugundua na Kuchunguza Ulaghai na Uhalifu Mwingine:** Kuzuia, kugundua, na kuchunguza ulaghai na uhalifu mwingine unaodaiwa kufanyika.
- **Kuthibitisha Utambulisho Wako:** Ili kulinda wewe na mali zako kwa kuthibitisha utambulisho wako.
- **Kwa Tathmini na Uchambuzi:** Kutathmini, kufanya majaribio (pamoja na majaribio ya mifumo) na uchambuzi (ikiwemo ukadiraji wa mikopo na/au tabia ya matumizi), uchambuzi wa takwimu, soko na bidhaa, na utafiti wa soko. [Tunaweza kutumia taarifa hii kuandaa ripoti za takwimu zinazoshirikiwa ndani ya kampuni yetu au kwa kampuni zetu za kundi. Tunakusanya ripoti hizi kutoka kwa taarifa zako na wateja wetu wengine. Taarifa hizi hazihusishi taarifa ya kibinafsi na huwezi kutambulika kutoka katika ripoti hizo.]
- **Kuthamini, Kuendeleza na Kuboresha Huduma Zetu:** Kuthamini, kuendeleza na kuboresha huduma

zetu kwako na wateja wengine.

- **Kulinda Maslahi ya Biashara Yetu na Kuendeleza Mikakati ya Biashara:** Kulinda maslahi yetu ya kibiashara na kuendeleza mikakati yetu ya biashara.
- **Kuwasiliana na Wewe:** Kuwasiliana nawe kwa barua, simu, ujumbe mfupi, barua pepe na njia zingine za kidijitali. Hii inaweza kuwa kwa sababu kama vile kukusanya madeni yoyote unayodaiwa kwetu.

MAAMUZI YANAYOFANYWA KIOTOMATIKI

Maombi yako ya bidhaa yanaweza kushughulikiwa kwa mchakato wa maamuzi ya kiotomatiki kama vile:

- Ukaguzi wa uwezo wa mkopo.
- Ukaguzi wa kudhibiti utakatishaji wa fedha na vikwazo.

KUSHIRIKIANA TAARIFA

Tunahifadhi taarifa zako binafsi kwa usiri mkubwa. Hata hivyo, ili kukidhi mahitaji yako na kukupa bidhaa na huduma bora zaidi, tunaweza kushiriki taarifa yoyote unayotupatia na kampuni nyingine ndani ya kundi letu, mawakala wao, washirika, na watoa huduma za usaidizi au wachakataji wa taarifa, popote walipo. Ikiwa umetupatia taarifa kwa wanachama wengine wa kundi letu, mashirika hayo yanaweza pia kushiriki taarifa hiyo nasi. Tutahakikisha kwamba kushiriki taarifa hiyo na wahusika wengine ni kwa kufuata sheria wakati wote.

Ili kusaidia kutoa huduma zetu, taarifa yako itachakatwa ndani na nje na wahusika wengine. Tunatumia wahusika wengine kwa ajili ya [usimamizi, utoaji wa huduma, ufuatiliaji na uhifadhi wa taarifa yako]. Tutaelekeza baadhi ya huduma kwa wahusika wa nje ambao tunawachukulia kuwa na uwezo wa kutekeleza shughuli za uchakataji zinazohitajika bila kupunguza kiwango cha huduma tunachokupa.

Wapokeaji wa taarifa zako, au makundi ya wapokeaji, yanaweza kujumuisha:

- Mamlaka za udhibiti zinazotekeleza majukumu yao kama vile Mamlaka ya Mapato na mashirika ya uchunguzi.
- Washirika wa malipo wanayotusaidia kuchakata uhamisho wa fedha ndani na nje ya nchi.
- Mashirika ya tatu yanayotusaidia kufanya tafiti za masoko.
- Wauzaji ambao benki huajiri kwa huduma za kusaidia biashara.
- Mtu yeyote ambaye tunaweza kuhamisha haki na/au wajibu wetu kwake.
- Mtu mwingine au shirika baada ya mabadiliko ya muundo, mauzo, au ununuzi, mradi mtu huyo anatumia taarifa zako kwa madhumuni yale yale ambayo ilikusudiwa awali au ilivyotumika nasi (au zote mbili).

- Ofisi za kumbukumbu za mikopo, mashirika ya kuthibitisha kitambulisho na anwani.

MAELEZO YA UHAMISHO WA TAARIFA NJE YA TANZANIA

Taarifa zako tulizonazo zinaweza kuhamishwa au kuhifadhiwa katika nchi nyingine nje ya Tanzania kwa madhumuni yoyote yaliyotajwa katika Notisi hii ya Faragha, ikijumuisha nchi ambazo zinaweza kuwa na sheria zinazotofautiana (na zinazoweza kuwa na kiwango cha chini cha ulinzi) kuhusu ulinzi wa taarifa binafsi. Hii ina maana kuwa taarifa hizo zinaweza kutii sheria na matakwa ya kufichua taarifa ya nchi hizo kwa madhumuni yoyote halali.

Tunapohamisha taarifa nje ya Tanzania, sisi au wahusika wengine walioidhinishwa tutahakikisha kuwa uhamisho huo ni halali, ruhusa kutoka kwa mwenye taarifa imetafutwa, kibali cha uhamisho kimepatikana kutoka kwa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC), na kuwa kuna kiwango kinachofaa cha ulinzi wa taarifa hizo.

UHIFADHI NA UONDOAJI WA DATA

Tutaifadhi tu taarifa tunazokusanya kuhusu wewe katika mifumo yetu au kwa watu wa tatu kwa makusudi yaliyotajwa hapo juu au kama inahitajika kwa mujibu wowote wa kisheria tunao paswa kutimiza.

Kwa kawaida, tutaharibu, kuhifadhi kwenye kumbukumbu, kupseudonimisha, au kufuta taarifa baada ya muda uliowekwa kisheria kuisha. Hata hivyo, tunaweza kuendelea kuhifadhi taarifa zako au taarifa zinazohusu akaunti yako hata baada ya wewe kuacha kuwa mteja, endapo itahitajika kwa madhumuni ya kisheria, ya udhibiti, ya kuzuia udanganyifu, au kwa sababu nyingine halali za kibiashara.

UHIFADHI WA TAARIFA YAKO NA USALAMA WA TAARIFA

Taarifa zote utakazotupa zinahifadhiwa kwenye seva zetu salama. Endapo tumekupa (au umechagua mwenyewe) nenosiri ambalo linakuwezesha kufikia sehemu maalum za tovuti yetu, wewe unawajibika kulinda usiri wa nenosiri hilo. Tunaomba usishiriki nenosiri lako na mtu yeyote.

Tumeweka hatua stahiki za kiusalama ili kuzuia taarifa zako binafsi kupotea kimakosa, kutumiwa au kufikiwa kwa njia zisizoidhinishwa, kubadilishwa, au kufichuliwa. Pia, tuna taratibu maalum za kushughulikia uvunjaji wowote unaoshukiwa wa usalama wa taarifa na tutakujulisha pamoja na mamlaka yoyote inayohusika endapo kuna uvunjaji tunapolazimika kufanya hivyo kisheria.

Tafadhali soma sehemu ya tovuti yetu inayohusu usalama mtandaoni ambayo unaweza kufikia kwa kubofya hapa: <http://equitygroupholdings.com/privacy-policy>.

MAWASILIANO YETU NA WEWE

Tunaweza kuwasiliana nawe kupitia barua pepe, posta, simu, ujumbe mfupi, na njia nyingine za kidigitali. Hatutawahi kukuomba nenosiri lako au namba ya akaunti yako.

Unapowasiliana nasi kupitia njia zozote za mawasiliano ikiwemo kutembelea tawi la benki au kupiga huduma ya simu, tutathibitisha utambulisho wako kwa kukuuliza maswali kadhaa kwa mujibu wa taarifa tunazomiliki kuhusu wewe na miamala kwenye akaunti yako. Tunaweza kurekodi simu zako kwa madhumuni ya mafunzo, ubora wa huduma, na usalama.

TAARIFA ZA MASOKO

Sisi na wanachama wengine wa kundi letu tunaweza kutumia taarifa zako kukufahamisha kuhusu huduma zinazoweza kukuvutia kwa barua, simu, meseji za simu, barua pepe au njia nyingine ya kielektroniki.

Unaweza kuomba tusitishie huduma kwa kukutumia ujumbe kwa njia moja wapo au zote muda wowote kwa kuwasiliana nasi kupitia mawasiliano yetu hapo chini.

Kama ungependa kuwasiliana nasi kuhusu haki zozote zilizoainishwa hapo juu, tafadhali wasiliana nasi kupitia barua pepe TZ-DPO@equitybank.co.tz au [wasiliana nasi](#). Kulinda faragha yako na usalama, tunaweza kuchukua hatua za kuthibitisha utambulisho wako kabla ya kukupatia maelezo yoyote.

HAKI ZAKO

Una haki kadhaa kuhusu taarifa tunazomiliki kukuhusu, zikiwemo:

- **Haki ya kupata taarifa zako za kibinafi tulizonazo**, kujua lengo la kuchakata taarifa hizo, na kufahamu kuhusu wachakataji wetu wa tatu.
- **Haki ya kuzuia ukusanyaji au uchakataji wa taarifa zako za kibinafi**; hata hivyo, tunaweza kuendelea kuchakata taarifa pale tunapokuwa na sababu halali za kisheria au sheria inapotutaka kufanya hivyo.
- **Haki ya kurekebisha taarifa zako**; kwa kurekebisha data ambazo ni za uongo au za kupotosha.
- **Haki ya Kufutwa kwa Taarifa (“haki ya kusahauliwa”)**; haki ya kuomba tufute data za uongo au za kupotosha kuhusu wewe. Una haki ya kuomba taarifa zote tulizonazo kuhusu wewe zifutwe, lakini tunaweza kukataa ombi hili endapo tuna sababu halali au tunatakiwa kufanya hivyo kisheria.
- **Haki ya kupinga uuzaji wa moja kwa moja**; una haki ya kujiondoa kutoka kwenye mawasiliano ya kibiashara yanayotumwa kwako kwa kupiga kituo cha huduma kwa wateja au kwa kututumia barua pepe: TZ-DPO@equitybank.co.tz

- **Haki ya kuzuia maamuzi ya kiotomatiki;** una haki ya kufahamishwa kuhusu maamuzi yoyote ya kiotomatiki au upimaji wa tabia unaofanywa kwenye data zako za kibinafsi unaoweza kuathiri kiwango cha huduma unachopokea. Pia una haki ya kupinga uchakataji wa aina hii; unaweza kutumia haki hii kwa kututumia barua pepe kwa: TZ-DPO@equitybank.co.tz au kuwasiliana nasi: [wasiliana nasi](#)

Kwa mawasiliano zaidi kuhusu haki zako, tafadhali wasiliana nasi kupitia dpotz@equitybank.co.tz au [wasiliana nasi](#) au tembelea tawi lolote karibu nawe.

TAARIFA HII YA FARAGHA

Yaliyomo katika Taarifa hii ya Faragha yanaweza kubadilishwa siku zijazo na mabadiliko yatachapishwa kwenye ukurasa huu.